

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**  
**15 Machi 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mwishehe  
Aseli Wilison  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Juma Ali Salehe Jongo  
Jumanne Idd Selemani  
Kassim Bakari  
Kibwana Mohammad Msiga  
Paulo Atibu Hatibu  
Protace Mugondo  
Sosthenes C Amlima  
Sudi Saidi Ramadhan

**Mkutano Temeke**

Jumamosi iliyopita Juma, Elaine, Paulo na Sudi Saidi walienda Temeke sokoni kuwaambia wapanda baisikeli kule kuhusu UWABA na kupata wanachama wapya. Wanachama wapya 41 walijiunga. Ili kuanzisha tawi kule lazima tuwe na wanachama ambao wako tayari kuendesha mikutano kule, basi tulipendekeza wanachama wa Temeke ambao watapenda kufanya kazi hii waje kwenye mikutano Mabibo mara mbili au tatu kwanza. Paulo alipendekeza pia tuende Kigamboni siku nyingine kwa sababu kuna wapanda baisikeli wengi kule.

**Mkutano na Halmashauri la Jiji, Barabara ya Morogoro, kodi ya baisikeli**

Wakati tulifuatalia jibu la barua yetu Halmashauri ya Jiji, Mama Mlamba alipendekeza kumtembelee kupata maelezo zaidi Jumatatu. Juma, Elaine, Paulo, Jumanne na Filbert walienda kutana naye. Alitupa jibu la barua yetu ambayo inasema tutaalikwa kwenye mazungumzo kuhusu mpango wa usafiri wa Dar es Salaam na majenzi ya barabara ya Morogoro, lakini barua haikuwa na jibu la maswali yetu maalum kama vipi njia za baisikeli zitalindwa ili magari hayawezi kuzitumia. Kwa ujumla yeche na idara yake wanapenda sana kuhamasisha wapanda baisikeli na wana mpango wa kujenga njia za baisikeli barabara ya Morogoro, na pia anapenda baisikeli za walemovu, lakini hapendi maguta. Elaine aliandika dondo za mkutano ule na tuliongeana kuhusu mkutano ule kwenye mkutano huu. Pia Juma alimletea dondo kwa Mama Mlamba wakati wa wiki.

Mama Mlamba alipendekeza tuombe kodi au ushuru ya kuingiza baisikeli nchini ipunguwe. Tuliamua kwanza tutafute taarifa kuhusu kiwango cha kodi na ushuru ambayo ipo, kabla ya kuomba Wizara ya Fedha ipunguzwe.

Vifuniko vya fereji zinazopita service road kwenye eneo la Jangwani barabara ya Morogoro vimeondolewa, labda wizi waliziiba. Hii inasababishwa wapanda baisikeli kushuka na kupanda tena baisikeli kila mara na ni shida kubwa kwa walemovu.

Wapanda baisikeli wengi wanatumia barabara kubwa kuepuka shida hii. Tuliamua kuandika barua TANROADS Dar es Salaam kuomba waweke vifuniko vipyta na waweke zege ili visiibiwe.

### **SUMATRA na matatizo ya wanafunzi kusafiri shulenii**

Gazeti la Citizen walikuwa na makala inayosema SUMATRA (Surface and Marine Transport Regulatory Authority) wanaandika repoti kuhusu matatizo ya wanafunzi kusafiri shulenii kwenye maeneo ya majiji kama Dar es Salaam. Elaine alitembelea ofisi zao na aliongea na David Mziray ambaye anaandika repoti. Alimwonyesha repoti ya draft lakini kuna masuala ya mabasi tu na siyo masuala ya baisikeli au hata kutembea kwa miguu. Lakini Elaine alipopendekeza aangalie masuala ya baisikeli kwenda shulenii aliona hili ni wazo zuri. Siku baada ya hapo Juma alimletea barua ambayo inaeleza faida za baisikeli kama usafiri kwenda shulenii kwa wanafunzi wanaokaa katika 10km kutoka shule na wana umri zaidi ya miaka 12, na ambayo inapendekeza vipi kuhamasisha wanafunzi waende shulenii na baisikeli na vipi kuhakakisha watakuwa salama.

### **Ofisi, guta na mambo ya hela**

Ally Saidi Mwishehe aliendelea kumletea hela ya guta kwa Juma kila wiki na Juma sasa ana Tsh 18,000 ya hela ya UWABA. Juma alinunua hooks kwa ajili ya kuweka kamba ili karatasi zisimame vizuri kwenye rafu. Tunahitaji kamba zaidi kwa sababu kamba ya sasa imefaa kwa rafu mbili tu siyo zote nne.

Mejah alipaka rangi ya nembo ya UWABA ofisini. Inapendekeza, lakini wanachama walisema jinsi ambavyo alama za kanisa na msikiti zipo kubwa sana inaonekana kwamba UWABA ni shirika la dini na inaweza kuleta machanganyikio. Wanachama waliamua kutoa alama ya msalaba na msikiti kutoka nembo ofisini. Sosthenes alisema atafanya hivi wakati wa wiki.

Kwa sababu nembo ni kwenye ukuta wa upanda wa kulia tuliamua kuweka bao la tangazo ya ziada kwenye ukuta wa nyuma. Ally Saidi Mohammed bado hajaweka. Jumanne alisema atafuatalia wakati wa wiki ili Ally afanye.

### **Wamba Memorial Fund**

Bado hatujapata email kutoka Wamba memorial fund. Elaine alimpigia simu mwenyekiti wa Wamba Memorial Fund merekani na aliacha message ya voicemail.

### **Shindano ya kuandika essay**

Tulikumbushana kuhusu shindano la kuandika essay la Ibike, na wanachama walisema watajaribu kupata watoto kuandika.